# CLASS 7 END TERM 3 DECEMBER 2021

# KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 - 15. Katika kila nafasi, umepewa majibu manne. Teua jibu mwafaka kujaza nafasi hizo.***

Katika ulimwengu tuishimo na hali ya maisha inavyobadilika ni vyema watoto wawe waongofu. Jukumu hili ni la mzazi. Mzazi __1__ kujenga msingi __2__ kwa mtoto wake __3__ nidhamu. Haifai __4__ mtoto akitenda hivi ama vile huku wazazi wenyewe wanafanya __5__. __6__ kumpata mzazi akimkanya mwanawe asivute sigara, asilewe ama asitukane watu __7__ yeye mwenyewe anafanya __8__ tena machoni __9__ mwanawe! Elewa hivi, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo na anapobebwa hutazama kisogo cha nina. Endapo basi tunawataka wana hawa wawe waongofu na kupambana na hali hii ngumu ya maisha, ni sharti kama ibada tuwe vielelezo bora kwao.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. anapasa | B. anapaswa | C. wanapasa | D. wanapaswa |
| 2. | A. thabiti | B. dhaifu | C. akali | D. mnyonge |
| 3. | A. kufunga | B. kuhusu | C. kulenga | D. kufanya |
| 4. | A. kumkemea | B. kumbembeleza | C. kumwamuru | D. kumwamrisha |
| 5. | A. hayo yaya | B. haya hayo | C. hawa hayo | D. yayo hayo |
| 6. | A. Ni kawaida | B. Inashtua | C. Si ajabu | D. Ni vigumu |
| 7. | A. ghalabu | B. ilhali | C. ingawa | D. mradi |
| 8. | A. kinyume | B. ungwana | C. hisani | D. ajabu |
| 9. | A. kwa | B. na | C. pa | D. mwa |

Sijali alikuwa mtundu na __10__ wa mapuuza. Alikuwa __11__ haambiliki __12__ hasemezeki. Kila mtu __13__ kumsemesha, alimtilia huku na __14__ kule. Alitokea kuwa mfano bora wa __15__.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. mwingi | B. mwenye | C. mpole | D. mengi |
| 11. | A. aidha | B. kama | C. daima | D. abadaan |
| 12. | A. bali | B. ila | C. wala | D. ingawa |
| 13. | A. alipojitahidi | B. anapojitahidi | C. amejitahidi | D. hujitahidi |
| 14. | A. kumtolea | B. kumtoa | C. kumtoka | D. kumtolesha |

15. A. cha kuvunjika hakina fundi
    B. pang'okapo jino pana pengo
    C. pavumapo palilie si kazi kudamirika
    D. chombo hakiendi ila kwa kafi

***Kutoka swali la 16 - 30, jibu kulingana na maelezo uliyopewa.***

16. Kigaro ni kwa polisi, jopo la waandishi na _____ la ngozi.
    A. chane
    B. msumbi
    C. robota
    D. numbi

17. Chagua jibu lililo la viunganishi tu
    A. Minghairi bighairi, halafu, wala
    B. Kisasi, akali, kidogo, hafifu
    C. kefle, chordo, ewaa, wallahi
    D. Upesi, kwa maringo, sana, kijeshi

18. "Nisingalienda nisingalimwahi tabibu." Ndiko kusema
    A. Sikuwahi tabibu maadamu nilienda.
    B. Kutoenda kwangu kulisababisha kutomwahi tabibu.
    C. Nilimpata tabibu kwa kuwa sikuenda
    D. Maadamu nilienda nilimwahi tabibu.

19. Ni methali gani kati ya zifuatazo inayoleta maana kwamba ukipuuza ushauri ipo siku utakuja kurudia nasaha hiyo?
    A. Mkataa pema pabaya pamwita.
    B. Aachaye kweli huirudia.
    C. Mdharau biu huibiuka yeye
    D. Mdharau mwiba huota tende.

20. Jaza pengo kwa tanakali ifaayo
    Fatuma alianguka topeni _____
    A. pwata
    B. puu
    C. parr
    D. pwa

21. Leta jiko hili na _____ litakalofaa kwa kazi hii.
    A. jinginelo
    B. mengineyo
    C. jingineo
    D. lingineyo

22. Kipi ndicho kinyume cha
Mzee aliamka mapema.
   A. Kijana aliamka mapema.
   B. Kijana alilala akichelewa.
   C. Shaibu alilala amechelewa.
   D. Ajuza alilala akichelewa

23. Chagua sentensi iliyoandikwa katika kauli ya kutendesha kati ya zifuatazo.
   A. Ukuta wote umepakika rangi.
   B. Chakula kilipikwa na wazee.
   C. Dawa za kulevya ni hatari kwetu.
   D. Aliambiwa aandike kwa hati nzuri.

24. Ni kivumishi kipi kinachoweza kuundwa kutokana na nomino ucheshi?
   A. Cheka   B. Kicheko
   C. Mcheshi   D. Chekesha

25. Msimu wa jua kali bila mvua huitwa________
   A. kipupwe   B. vuli
   C. masika   D. kiangazi

26. **Upi ndio ukubwa wa:**
Mbwa wa mtu huyo ni mkali sana.
   A. Majibwa ya majitu hayo ni makali sana
   B. Jibwa la jitu hilo ni kali sana
   C. Kijibwa cha kijitu hicho ni kikali sana
   D. Vijibwa vya vijitu hivyo ni vikali sana

27. Nomino **'mali'** lipo katika ngeli gani?
   A. YA - YA   B. I - I
   C. U - YA   D. LI - YA

28. Onyesha maana ya maneno yaliyopigiwa mstari.
Zeituni na Zainabu ni **kinu na mchi.**
   A. hupendana sana
   B. hupenda kutembea bila kutulia
   C. hugombana kila mara
   D. hupenda kusaidiana kwa kila jambo

29. Nahau yenye maana ya kufanya kazi ngumu ni
   A. meza mate machungu
   B. kazi ya kijungujiko
   C. kazi ya sulubu
   D. kazi ya ujima

30. **Kanusha:**
Ukija utanipata.
   A. Ukija hutanipata
   B. Usipokuja hutanipata
   C. Ukienda utanikosa
   D. Usingekuja usingenipata

***Yasome makala yafuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Hivi majuzi Wizara ya Usalama ilitangaza mikakati yake ya kukabiliana na changamoto za kiusalama nchini kuanzia mwezi huu hadi wakati wa uchaguzi mkuu ujao. Miongoni mwa mikakati hiyo ni kukabiliana na utovu wa usalama katika kipindi cha kampeni za 2022, pamoja na kikosi maalum cha kupambana na utekaji nyara.

Japo waziri wa usalama Bw. Simba alipuuzilia mbali kina cha visa vya utekaji nyara nchini, ni hatua ya kutia moyo kuwa aliunda kikosi hicho. Kusema kweli ingawa mkuu huyu wa wizara alitilia shaka kukita mizizi kwa visa hivi nchini, ripoti za vyombo vya habari na mitandao inapozingatiwa, hakika visa vya watu kupotea vimekuwa foko nchini katika siku za hivi punde kuliko wakati mwingine wowote.

Wakati shule zinafungwa ndipo ilipo hatari. Hapa vyombo vya dola na vikosi vyote vya usalama sharti vikae ange kukomesha visa hivyo kutokea. Vikosi vya usalama vihakikishe vimeunda mikakati anuai na kabambe ya kuripoti mara moja tukio lolote la utekaji nyara mbali na kuchukua hatua za haraka kuhakikisha kuwa wahalifu hao wamebambwa.

Kwa sababu ya matarajio hayo ya kuongezeka kwa uovu huo ambao umekuwa tatizo sugu, sharti kila mmoja awe makini zaidi kutibua matukio ya aina hiyo.

Waama, hilo ni jukumu la kila Mkenya wala halipaswi kuachiwa vyombo vya usalama pekee. Naam, vikosi vya usalama vina wajibu mkubwa wa kutekeleza, maadamu ndivyo vilivyopewa nafasi kubwa na ya kimsingi ya kudumisha usalama. Hata hivyo kila raia kindakindaki na aliye mzalendo wa kweli, na wazazi wanaombwa kuwapa watoto wao tahadhari dhidi ya wahalifu hao waliojaa nchini kwa sasa.

Watoto wakanywe kuchukua zawadi zozote kutoka kwa watu wasiowajua pamoja na kukataa usaidizi wowote kutoka kwa watu wa sampuli hiyo.

Serikali itakuwa imesaidia pakubwa iwapo itatoa mwongozo unaoweza kuwasaidia wazazi na walezi kuwapa watoto wao mafunzo ya kukabiliana na tatizo hilo sugu. Aidha ni muhimu jinsi wizara ya usalama ilivyosema kuwa, taifa linapoelekea katika uchaguzi mkuu, pana uwezekano mkubwa wa visa hivi vya utovu wa usalama kuzidi na hivyo basi kuwepo haja ya kubuni mikakati madhubuti kuvizuia mapema.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

31. Kulingana na aya ya kwanza
A. serikali haijakuwa ikiweka mikakati ya kudhibiti usawa isipokuwa sasa.
B. visa vya utovu wa usalama huzidi wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu
C. utekaji nyara hutokea tu wakati wa kampeni
D. vyombo vya usalama huwa na wakati mgumu tu kampeni zinapofanywa

32. Mikakati iliyoundwa na wizara ya usalama ni idhibati kuwa
A. serikali imejiandaa kikamilifu kukabiliana na wahalifu
B. vyombo vya dola vimetepetea katika juhudi za kukomesha uhalifu
C. wizara husika ndio sasa imegundua kuwa utekaji nyara umekita mizizi
D. awali hapakuwa na haja kwani hakukuwa na uhalifu wowote

33. Waziri wa usalama...
A. anatilia shaka uwezo wa kikosi chake kupambana na uhalifu
B. hakubaliani na taarifa kuwa uhalifu umezidi nchini
C. hana hakika iwapo vipo visa vyovyote vya uhalifu nchini
D. anaziunga mkono taarifa za vyombo vya habari na mitandao kuwa hakuna uhalifu nchini

34. Katika siku za hivi karibuni kulingana na vyombo vya taarifa na mitandao, visa vya watu kupotea
A. vimepungua sana
B. havijakuwa vikitokea
C. vimekuwa vikitokea kwa uchache mno
D. vimezidi kuliko wakati wowote

35. Visa vya uhalifu vinatarajiwa kuzidi wakati gani?
A. Wanafunzi wanapofungua shule.
B. Kipindi wanafunzi wanaendelea na masomo yao.
C. Kampeni zinapositishwa nchini.
D. Wanafunzi wanapokuwa likizoni.

36. Ni maelezo yapi yaliyo sahihi kwa mujibu wa taarifa?
A. Wanahabari ndio tu wanaostahili kuripoti visa vya uhalifu
B. Ni jukumu la polisi pekee kutuhakikishia usalama wetu.
C. Mwananchi yeyote mzalendo hana haki kisheria kupigania usalama wake
D. Ili tuwe salama sote lazima tuwajibike

37. Wazazi wameombwa kufanya nini ili kuwahakikishia watoto wao usalama?
A. Kuwatahadharisha watoto dhidi ya uhalifu.
B. Kuwakamata wahalifu wakati wowote.
C. Kuripoti tu visa vya uhalifu kwa polisi.
D. Tuwakamate na kuwaua wote wanaotekeleza uovu.

38. Watoto wakanywe dhidi ya
A. kutumwa dukani ovyoovyo
B. kuwasalimia watu wowote
C. kupokea zawadi ama kuomba usaidizi kwa wasiowajua
D. kuripoti visa vyovyote kwa wazazi wao

39. Serikali katika aya ya mwisho inaombwa
A. kutoa mwongozo wa kusaidia wazazi.
B. kuwatia wazazi moyo ili wapambane na uovu.
C. kuwashtaki wazazi wasioripoti visa vya uovu.
D. kutowatuma wanao ovyo madukani na sokoni.

40. Neno madhubuti limepigiliwa mstari. Lina maana kuwa
A. iliyo ngumu
B. isiyotikisika
C. isiyotakikana
D. isiyosaidia sana

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali 41 - 50***

Sikubahatika mama, kufanya ulivyotaka,
Kwa bidii sikusoma, mdaraja kuuvuka,
Mtimani yaniuma, sana nimesononeka,
Sikubahatika ila, nitajaribu mwakani.

Sikubahatika baba, nisamehe tafadhali,
Likuwa kali dhoruba, nilijaribu kwa kweli,
Siyapunguze mahaba, nipende kama awali,
Sikubahatika ila, nitajaribu mwakani.

Sikubahatika dada, kuhepa kuwaangusha,
Kulifanya la ziada, ili kuwafurahisha,
Sio yangu kawaida, mie kuwahuzunisha,
Sikubahatika ila, nitajaribu mwakani.

Sikubahatika ila, nitajaribu mwakani,
Na nimevunjika ila, sifi moyo asilani,
Nahuzunika ila, sijachoka masomoni,
Sikubahatika ila, nitajaribu mwakani.

Nitajaribu mwakani, bado nina nyingi nguvu,
Msiache kuniamini, damuni sina uvivu,
Sijachoka akilini, niombeni utuvu,
Sikubahatika ila, nitajaribu mwakani.

Niombeeni salama, niombee kwa Jalali,
Nisije kukata tama, yajapo mambo makali,
Kupambana sitakoma, naapa sili silali,
Sikubahatika ila, nitajaribu mwakani.

**41.** Shairi hili ni la bahari gani?
- A. Tathlitha
- B. Tarbia
- C. Takhimisa
- D. Tasdisa

**42.** Mshairi anaomba nini kwa jamaa yake?
- A. Kuhurumiwa kwa kutofanya vizuri masomoni.
- B. kusamehewa kwa kutofanya vyema masomoni
- C. Kukashifiwa kwa kufeli mtihani
- D. Kusifiwa kwa kufeli mtihani

**43.** Mwandishi anamwomba baba yake
- A. asiache kumpenda
- B. asizidi kumpenda
- C. ampende japo kwa kadri
- D. asimpende asilani

**44.** Mshairi anasema kuwa alianguka mtihani kwa kuwa
- A. hakuwa amejiandaa vizuri
- B. mtihani ulichelewa kufika
- C. mtihani ulikuwa mgumu
- D. hakuweza kumaliza kuufanya

**45.** Ni kweli kusema kuwa
- A. mwandishi alikuwa mvivu
- B. wazazi na maumbu zake wamemgeukia kwa kuanguka mtihani
- C. tayari ameshaikata tamaa ya kuendelea na masomo
- D. daima yeye hupenda kuwafurahisha jamaa yake bali si kuwahuzunisha

**46.** Yaelekea mwandishi
- A. ana nia ya kujaribu tena
- B. hana haja ya kurudi shuleni tena
- C. masomo tayari yamekuwa mzigo kwake
- D. ingawa amehiari kurudi shuleni, hana ari ya kusoma kwa bidii

**47.** Mloto wa ubeti wa nne ni
- A. Sikubahatika ila, nitajaribu mwakani
- B. Na nimevunjika ila, sifi moyo asilani
- C. Nahuzunika ila, sijachoka masomoni
- D. Msiache kuniamini, damuni sina uvivu

**48.** Mshororo wa mwisho wa kila ubeti wa shairi hili huweza kutajwa kuwa
- A. kituo
- B kimalizio
- C. kiishio
- D. kiitikio

**49.** Ni idadi ngapi ya mizani iliyopo katika ubeti wa mwisho wa shairi hili?
- A. 64
- B. 16
- C. 8
- D. 128

**50.** Mtunzi wa mashairi huitwaje?
- A. Manju
- B. Sogora
- C. Malenga
- D. Mghani